Uzinduzi wa

MKAKATI WA TAIFA WA HIFADHI NA USIMAMIZI KAMILIFU WA MAZINGIRA YA PWANI

Dira ya Maisha Bora Pwani

Coastal Resources Center
University of Rhode Island

Tanzania Coastal Management Partnership

Uzinduzi wa

MKAKATI WA ICM WA TAIFA

Jumatano 16, 2003

Maandalizi ya Mkakati wa Taifa wa ICM

Maandalizi ya Mkakati wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (ICM), yalifanywa kwa utaratibu uliokuwa wazi na wa ushirikishwaji uliochukua zaidi ya miaka minne. Maandalizi yalizingatia maoni ya sekta zote na wahusika wote katika shughuli za pwani na amabayo yalibainisha umuhimu wa kuwa na utaratibu na mipango bayana ya usimamizi wa mazingira ya pwani. Pia Mkakati wa ICM umejengwa kwa misingi ya kisayansi na teknolojia. Zaidi ya nyaraka thelathini za nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na mambo ya kisayansi, sheria, uchumi, elimu na nyinginezo zimeandaliwa na wataalamu na kutumiwa kama vielelezo vya awali katika maandalizi ya Mkakati wa ICM.

Kazi ya kuandaa mkakati huu ilianza mwaka 1998 kwa kuunda kikundi cha wataalamu chenye wajumbe ishirini kutoka sekta mbalimbali (ikiwa ni pamoja na sekta binafsi), ili kubainisha masuala yanayohusiana na hifadhi na usimamizi wa pwani ya Tanzania. Kikundi hiki kilianza kwa kukusanya, kuchambua na kusanisi taarifa iliyopo ya ndani na nje ya nchi. Baadaye, kikundi kilitumia miezi kadhaa kutembelea wilaya zote za pwani na kufanya mazungumzo na watumishi wa serikali pamoja na wananchi.

Masuala yaliyokusanywa yaliwasilishwa kwenye mkutano wa Wakurugenzi na Makamishena wa sekta mbalimbali mwezi Oktoba 1998, ambao uliridhia juhudi zilizokuwa zinafanywa. Baada ya hapo, kikundi kilirudi tena kwenye wilaya na vijiji kwenda kuandaa dira, kanuni na mikakati ya kushughulikia masuala hayo. Mapendekezo ya kikundi cha wataalamu yaliwasilishwa na kuthibitishwa kwenye mkutano wa Wakurugenzi wa Mei, 1999.

Baada ya mkutano huo kikundi kilitayarisha rasimu ya mapendekezo ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maeneo ya Pwani, utekelezaji wake, mifumo ya utekelezaji na miundo ya usimamizi. Rasimu hiyo ilifanyiwa uhakiki Mwezi Septemba 1999 na vikundi vya wataalamu pamoja na wawakilishi wa programu tano za hifadhi na usimamizi wa pwani, katika mkutano wa siku tatu.

Waraka wa Mapendekezo ya utekelezaji sera na mifumo ya miundo ya usimamizi uliwasilishwa kwa mkutano wa kitaifa uliowajumuisha wabunge, wakuu wa wilaya, makatibu tawala wa mikoa, wkurugenzi wa halmahauri za wilaya, wakurugenzi na makamishena wa idara za serikali na wakuu wa taasisi za serikali katika mkutano wa siku mbili uliofanyika mwezi Novemba 1999. Mkutano huo ulipitia waraka huo na kuchagua mfumo wa utekelezaji na usimamizi wa sera ya ICM na kutoa maelekezo muhimu ya kuandaa rasimu ya awali ya sera.

Maelekezo na mapendekezo ya mkutano huu yalifanyiwa kazi na rasimu ya sera ya ICM kutayarishwa na kutawanywa kwa wadau ili kupata maoni zaidi kabla ya rasimu hiyo haijawasilishwa serikalini.

Serikali ilipitia kwa makini rasimu hiyo ya sera, na baadaye kushauri rasimu hiyo ibadilishwe katika muundo na mfumo wa mkakati unaolenga utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira. Wataalamu waliyazingatia maelekezo hayo, na wakaandaa rasimu ya Mkakati wa ICM ambayo uliwasilishwa serikalini na kuridhiwa. Katika mantiki yake Mkakati wa ICM unaziunganisha sekta mbalimbali na kuweka ushirikiano kamilifu wa kutumia, kusimamia na kuendeleza mazingira ya pwani na rasilimali zake kwa uendelevu.

Wakurugenzi wa sekta mbalimbali wakichambua maswala ya ICM katika mojawapo ya mikutano ya maandalizi ya Mkakati wa ICM

MAJUKUMU MAKUU YA ICM

Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (ICM) umeundwa katika maumbile na mfumo unaotoa fursa za utekelezaji wa vitendo halisi ambavyo vinapimika. Hii ni kutokana na muundo wa utekelezaji wa mkakati huo unaotoa fursa kwa wadau wote kushiriki katika hatua zote za utekelezaji, kuanzia kubainisha masuala ya kushughulikia, kuchagua na kupanga hatua za kuchukua, kutekeleza hatua hizo na kupima mafanikio katika kufanikisha malengo na majukumu makuu yafuatayo:

1. Kusaidia upangaji wa kimazingira katika shughuli za usimamizi kamilifu wa rasilimali za pwani katika ngazi ya wilaya na kuweka wazi taratibu za kuwainisha maslahi ya taifa na manufaa ya wananchi
2. Kuendeleza mbinu kamilifu na endelevu zinazofaa kimazingira za maendeleo ya matumizi makubwa ya kiuchumi ya rasilimali za pwani ili kupata manufaa ya juu kabisa
3. Kuhifadhi na kurejesha hali ya asili ya mazingira tekechu na maeneo yaliyo na ukwasi mkubwa wa bioanuwai na wakati huohuo kuhakikisha kuwa wakazi wa pwani wanaendelea kunufaika na matumizi endelevu ya rasilimali
4. Kuanzisha utaratibu wa hifadhi na usimamizi kamilifu wa maeneo ya pwani yaliyo na manufaa makubwa ya kiuchumi na/au yaliyo na uwezekano mkubwa wa kupata majanga ya asili
5. Kuandaa na kutumia utafiti wa mifumoikolojia ya pwani, na mfumo wa tathmini na ufuatiliaji unaofaa kuwezesha taarifa iliyopo ya kisayansi na kiufundi kutumika katika utoaji maamuzi ya hifadhi na usimamizi kamilifu
6. Kutoa fursa zinazofaa za kuwahusisha wadau katika mchakato wa maendeleo ya pwani na utekelezaji wa sera za usimamizi wa maeneo ya pwani
7. Kujenga uwezo wa watu na taasisi ili kuwezesha ushiriki wa taaluma na sekta mbalimbali katika usimamizi wa mazingira ya pwani

Uzoefu wa kimataifa katika utekelezaji wa ICM

Na Lynne Zeitlin Hale

Toka enzi na enzi, watu waishio ufukoni mwa bahari na kutumia rasilimali za bahari na pwani, wamekuwa na mfumo, aidhuru usiwe mzuri, wa kusimamia rasilimali za pwani. Mara nyingi wenyeji wa pwani, wamekuwa na taratibu zao zinazowasaidia kusimamia rasilimali hizo kwa manufaa ya watu kwa muda mrefu, ingawa mifumo hiyo haipangwi kwa malengo ya kuweka misingi ya kiutwala.

Mabadiliko makubwa ya usimamizi wa rasilimali za pwani yalianza katika karne za 19 na 20 kutokana na kuongezeka kwa watu na kuwepo mabadiliko makubwa ya tekelenojia. Majukumu ya usimamizi yalichukuliwa zaidi na serikali na hivyo katika nchi nyingi, watu wakawa na uhuru wa kutumia bahari wapendavyo. Hali hii ilipelekea uvurugaji wa mazingira na upotevu wa rasilimali licha ya kusababisha migongano katika matumizi.

Hali hii ndiyo iliyopelekea kuanzishwa kwa ICM ambayo sasa inatambuliwa na Umoja wa Mataifa kama chombo mahususi ambacho kinalenga kuboresha maisha ya watu ambao wanategemea rasilimali za pwani, wakati huohuo wakijibidisha kulinda na kuendeleza ikolojia ya pwani kwa uzalishaji zaidi.

Kufuatana na na tafsiri ya ICM ya Umoja wa Mataifa, ICM ni utaratibu endelevu unaoiunganisha serikali na wananchi, sayansi na utawala, sekta na umma katika kuandaa na kupanga mipango kamilifu ya kulinda na kuendeleza mazingira ya pwani na rasilimali zake.

Tofauti na mipango mingine ya usimamizi wa maeneo ya pwani, programu za ICM mara nyingi huzingatia eneo la pwani na watu wanaoishi katika eneo hilo ili kuwa na 'dira ya maisha bora', na kisha kuweka mikakati inayowahusisha wadau wote ili kupata maisha bora. Katika kutekeleza ICM, shughuli za maendeleo pwani husimamiwa kikamilifu ili kupata manufaa zaidi na wakati huohuo juhudi zikifanywa kuepuka athari za sekta moja kuielemea nyingine.

Lynne Hale ambaye alitoa mchango mkubwa katika maandalizi ya Mkakati wa ICM

Misingi na nguzo muhimu za mafanikio ya ICM ni pamoja na kuwapa fursa wahusika wote 'kumiliki' programu ya ICM. Hii ni pamoja na serikali kuitambua programu ya ICM na kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali; ushiriki wa wadau wote; na upatikanaji wa msaada endelevu kutoka kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za wafadhili.

Muhimu pia ni wadau kushiriki kikamilifu katika hatua zote za uanzishaji hadi utekelezaji wa programu ya ICM. Hii huwapa fursa wadau sauti na uwezo wa kufanya maamuzi kulingana na tamaduni na mila zao.

Nguzo nyingine ya mafanikio ya programu ya ICM ni kuwa na mikakati inayofanikisha kupata malengo yaliyokusudiwa. Hii inatokana na ukweli kwamba haiwezekani kuwa na programu, hata kama ni kamilifu vipi, ambayo inaweza kuyakabili na kuyatatua masuala yote yanayohusika na usimamizi wa mazingira ya pwani. Hivyo, ili kuwa na mikakati ya utekelezaji yenye malengo ni muhimu kuyapanga masuala kufuatana na uzito wa matatizo yake. Hii itatoa fursa ya kulikabili suala baada jingine kwa mafanikio zaidi.

Sambamba na hilo, programu ya ICM husaidia kuweka utekelezaji ulio 'kamilifu', ambao husaidia kuweka uwiano baina ya ngazi za juu za utawala na ngazi za chini za wananchi. Hii hutoa fursa kwa vyombo vya juu vya serikali kuwajibika kwa kutoa miongozo na sera ambazo huwaongoza wananchi katika kuleta mabadiliko.

Pia utekelezaji kamilifu huusisha sekta mbalimbali, utaratibu ambao husaidia kutatua masuala magumu ya sekta moja kuielemea sekta nyingine kutokan na matumizi ya rasilimali na mazingira. Utaratibu huu pia huzingatia matumizi ya sayansi katika usimamizi, ili kuelewa vyanzo vya matatizo katika ikolojia na kupata ufumbuzi. Katika mantiki yake, ICM au hifadhi na usimamizi kamilifu ni utaratibu endelevu na siyo utaratibu wa kutatua tatizo kwa njia za zima moto na kuacha.

Na kutokana na uzoefu katika nchi nyingi, hakuna 'fomula' au jawabu moja katika usimamizi wa mazingira ya pwani. Kila taifa na kila eneo huwa na matatizo yake ambayo hutatuliwa kwa utaratibu wake. Ni kutokana na kujifunza kwa kutenda kwamba wasimamizi wa mazingira ya pwani wataweza kubainisha njia zipi zitaleta au hazitaleta mafanikio katika nchi au eneo linalokusudiwa.

TIMU YA UHARIRI
Gratian Luhikula
Joe Nakajumo
Tuma Abdallah
Muhingo Rweyemamu
Pudenciana Temba

Kauli ya Waziri wa Nchi (Mazingira) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mh. Arcado Ntagazwa (MB)

Tanzania imebahatika kuwa na bahari. Pwani yetu yenye mandhali ya kuvutia ni sehemu muhimu sana ya mazingira yenye rasilimali nyingi. Pwani na bahari yake ina mifumo mingi ya ikolojia-asili, yakiwemo matumbawe, fuko, milango ya mito, nyasi bahari na misitu ya miti ya mikoko. Vyote hivi ni urithi mkubwa, ambao ni mhimili wa maisha ya watu.

Kutoka Tanga hadi Mtwara, pwani yenye urefu wa zaidi ya kilomita 800 ina umuhimu wa pekee katika maendeleo ya taifa na maisha ya wakazi wa pwani. Ina fursa tele za kijamii na kiuchumi. Hizi ni pamoja na uchukuzi na usafirishaji kwa meli, uvuvi, utalii, biashara, kilimo, makazi ya watu na viwanda, achia mbali ufugaji viumbe bahari na uchimbaji wa gesi - nyanja za kiuchumi zinazoanza kushamiri. Fursa hizi za kiuchumi zina uwezo wa kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuboresha maisha ya wakazi wa pwani na Watanzania kwa ujumla.

Pamoja na manufaa hayo muhimu, pwani ni mfumo wa kipekee ambamo mambo kadhaa yanapaswa kuzingatiwa kwa makini, yakiwemo yale yanayohusiana na bionuai, uchumi, jamii na taasisi, ambayo ni lazima yaainishwe katika mfumo wa usimamizi ambao unaleta manufaa bila kuleta madhara katika mazingira nyeti ya pwani.

Hii ndio changamoto inayoikabili Tanzania kuwa na utaratibu utakaotuongoza vyema kusimamia na kutumia rasilimali za pwani kwa uendelevu. Tunahitaji chombo ambacho kitatupa dira ya kufanikisha kuendeleza rasilimali za pwani na baharini ili tuweze kuainisha maendeleo na hifadhi.

Utaratibu na chombo ambacho kitatuhakikishia mafanikio hayo ni Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani (ICM), ambao tunauzindua. Mkakati huo utatuongoza kupata maendeleo endelevu kutokana na ushirikiano baina ya serikali na wananchi, sayansi, na sekta mbalimbali katika ngazi ya taifa hadi vijijini tukizingatia misingi ya kuendesha mambo kisayansi.

Kwanini tumechagua ICM? Tanzania, kama zilivyofanya nchi nyingine nyingi zenye pwani, imechagua ICM kwa sababu nyingi nzuri. ICM ina sifa za pekee. Licha ya kusaidia katika kupanga vyema utekelezaji wa shughuli, hubainisha mapungufu katika kuyatatua masuala magumu ambayo husababisha migongano ya usimamizi na matumizi miongoni mwa sekta mbalimbali. ICM hutumika kama 'msuluhishi' wa masuala mbalimbali na 'kiungo' wa wadau, wakiwemo wafanya maamuzi, watekelezaji na watumiaji.

Ni matumaini ya Serikali kwamba Mkakati wa ICM ukitekelezwa vyema, Tanzania siyo tu itafanikiwa kuyakabili masuala magumu ya usimamizi yanayosababisha matumizi yasiyoendelevu, bali itaweza kusimamia rasilimali za pwani kwa uendelevu na kwa manufaa mazuri zaidi. Hii itasaidia watu waliopo leo na wa vizazi vijavyo kunufaika na rasilimali za pwani.

Mantiki ya Mkakati wa ICM ni kwamba unatekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ambayo inaunganisha sekta zote katika ngazi ya wilaya na kuweka usimamizi wa pamoja katika kuleta maendeleo endelevu. Ingawa zipo sera za sekta mbalimbali za kuongoza matumizi na maendeleo ya rasilimali, wakazi wa pwani, hasa wale wa vijijini wanaendelea kuwa masikini. Watu hawa wanahitaji kuongozwa vyema ili waweze kujinasua katika janga la umasikini na wakati huohuo wao wenyewe wakiwa mashahidi wa kujibidisha kuyahifadhi mazingira kwa uzalishaji zaidi kwa manufaa yao.

Ni matarajio na kusudio la serikali kutumia kikamilifu nguzo za Mkakati wa ICM kuboresha jinsi ya kufikia mchakato na maamuzi yanayolenga maendeleo endelevu, kwa kutoa ufafanuzi na mwongozo wa matumizi pamoja na mgawanyo wa rasilimali katika ngazi ya taifa hadi vijijini. Hii itafikiwa kupitia muundo wa utekelezaji wa ICM ambao unaziunganisha sekta mbalimbali ili kuwepo maamuzi ya pamoja juu ya usimamizi wa rasilimali unaozingatia hifadhi ya mazingira, msingi wa rasilimali zote-resource base. Kutokana na utekelezaji mzuri wa ICM, serikali inaamini kwamba wananchi, hasa wanaoishi pwani watapata fursa ya kuboresha maisha yao.

Mkakati wa ICM pia utachangia katika juhudi za kuhifadhi viumbe muhimu na mazingira yake. Aidha, mkakati utasaidia katika usimamizi wa maeneo yenye umuhimu wa kiuchumi na maeneo yaliyo katika mazingira tekechu ambayo mara nyingi hukumbwa na masahibu yanayosababishwa na matukio ya asili. Kulifanikisha hili, utafiti wa kisayansi,

Mh. Arcado Ntagazwa

ufuatiliaji na ukadiriaji wa mabadiliko utatumika kikamilifu ili kusaidia kufanya maamuzi ya usimamizi.

Hivyo, maamuzi ya kuweka Mkakati wa ICM ni maamuzi ya busara. Ni matumaini ya serikali kwamba Mkakati huu utatekelezwa kwa ufanisi ili uwe 'dira ya maisha bora' kwa wakazi wa pwani. Utakuwa mwenge wa kutuangazia katika maisha ya mbele, ambamo rasilimali za pwani zitasimamiwa kikamilifu ili kupata manufaa zaidi katika sekta mbalimbali na wakati huo huo tukiepuka athari sa sekta moja kuilemea nyingine.

Mkakati huu wa ICM ni njia muafaka itakayotufikisha kwenye maisha ya matumaini. Maisha yenye watu wenye uhakika na hali ya maisha yao na wenye makazi mazuri, ambao kwa pamoja wanashirikiana kulinda na kuendeleza maeneo ya pwani na rasilimali zake kwa manufaa yao wenyewe na kwa manufaa ya taifa letu kwa jumla.

Kauli ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Magnus Ngoile



Dk. Magnus Ngoile,

Mwanamazingira mmoja, Henry David Thoreau aliwahi kuuliza swali lenye busara: "Kuna busara gani kuwa na nyumba nzuri ikiwa huna ardhi nzuri ya kuiweka?" Na huenda ni kwa busara kama hiyo, mwaka 2000 watu wa Rufiji walikataa mradi wa ufugaji kamba, ambao ulinadiwa kama mkombozi wa maisha ya watu wa Rufiji na vizazi vyao vijavyo.

Watu hao wa Rufiji walijua faida na manufaa ya mradi wa kamba. Lakini walihitaji wahahakikishiwe kwamba mradi huo usigeleta madhara katika mazingira ya bonde lao. Kwa bahati mbaya, mwekezaji hakuweza kutoa jibu la kuridhisha. Na hivyo wakazi wa Rufiji wakaamua kutokuwa na 'nyumba' kuliko kuwa na nyumba isiyokuwa na msingi imara.

Msimamo huo wa watu wa Rufiji unastahili kupongezwa, kwani kuna watu wengi duniani ambao hawana uwezo na fursa ya kutetea haki zao. Hali hii hupelekea kufanyika kwa miradi ambayo matokeo yake ni kuchafua na kuharibu mazingira na hatimae kuyavuruga kabisa maisha ya watu.

Mfano mzuri ni mradi wa bwawa la Akosombo nchini Ghana lililojengwa katika mto wa Volta kati ya mwaka 1950 na 1960. Kikubwa kilichopatikana kutokana na mradi huo, ni watu zaidi ya 100,000 wanaoishi kandokando ya mto kupata maradhi ya macho, na zaidi ya watu 70,000 miongoni mwao kupofuka kabisa kutokan na virusi vilivyotokana na bwawa hilo. Watu wengine 80,000 wamepata vilema vya kudumu kutokana na maradhi yajulikanayo kama schistosomiasis ambayo yalisababishwa na aina ya konokono ambao walianza kuzaliana kwa wingi katika bwawa hilo.

Matatizo ya mazingira ni agenda kuu ya ulimwengu wa sasa. Tatizo la mazingira linaenda sambamba na kuongezeka kwa watu kwa kasi kubwa kunakoambatana na utandawazi. Masuala yanayoambatana na matatizo ya mazingira ni pamoja na uharibifu wa ardhi, uchafuzi wa hewa na maji na uharibifu wa maliasili. Kila tatizo linatishia uhai na maendeleo ya watu kiuchumi.

Mazingira yasiyotunzwa na kuhifadhiwa ni sawa na kutokuwepo. Na ndiyo maana napenda kutumia fursa hii kuishukuru na kuipongeza serikali kwa kuchukuwa hatua za makusudi za kuweka mikakati ya kuyahifadhi na kuyalinda mazingira, hasa mazingira ya pwani.

Mkakati wa Taifa wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani utatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Tanzania. Utaiunganisha serikali na wananchi, sayansi na utawala, watu na sekta mbalimbali katika mpango wa kulinda na kuendeleza mazingira na rasilimali za pwani. Mbali na kuyalinda mazingira, mkakati huu pia utalenga kuboresha maisha ya watu.

Ni jambo lililo wazi kwamba mikoa iliyopo pwani, Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara huchangia theluthi moja ya pato la taifa, lakini wakazi wa mikoa hiyo ni masikini sana. Makadirio ya sasa ya wastani wa mapato wa wananchi wa mikoa ya pwani ni chini ya shilingi 100,000/- kwa mwaka.

Lengo la Mkakati wa ICM ni kubadili hali ya shughuli za kiuchumi. Nia ni kuwawezesha watu kufanya shughuli za kiuchumi zaidi ya moja, ili shughuli moja isipokwenda vyema, jamii au familia iwe na njia nyingine ya mapato na chakula.

Jukumu la ICM ni kuweka uwiano ili kuepuka madhara ya kiuchumi na mazingira ambayo baadhi yake yamekwisha anza kuharibiwa kutokana na vitendo mbalimbali, vikiwemo ukokotaji wa kamba, uchimbaji matumbawe kwa ajiri ya ujenzi, na uendeshaji wa viwanda usioendelevu.

Hakuna shaka kwamba viwanda huleta manufaa mengi yakiwemo ajira, maisha mapya na uhusiano wa kimataifa. Lakini inatubidi tuwe makini na teknolojia ambayo mara nyingi hutoka katika nchi zilizoendelea.

Nchi hizo zilizoendelea, kwa mfano hutumia zaidi nishati na maliasili kuliko nchi zinazoendelea. Matokeo yake matatizo ya mazingira katika nchi zilizoendelea husababishwa na viwanda, matumizi makubwa ya maliasili na mahitaji makubwa ya vifaa na huduma.

Kwa upande mwingine, matatizo ya mazingira katika nchi zinazoendelea, husababishwa hasa na umasikini, ambapo kipaombele huwekwa katika kukimu maisha na si kuhifadhi mazingira. Na hii ndiyo sababu inayopelekea wawekezaji wa nchi zilizoendelea kupenda kuwekeza katika nchi zinazoendelea ambazo mazingira yake bado yamo katika hali nzuri.

Ndiyo maana nazipongeza juhudi za serikali katika kuweka utaratibu wa ICM, ambao utatupa fursa nyingi za kuyatumia mazingira ya pwani kwa uendelevu. ICM itatuongoza vyema, hasa wakati huu ambapo miradi ya maendeleo inaelekezwa katika maeneo ya pwani. ICM itatupa fursa ya kuchagua miradi, siyo kwa ukubwa wake, bali kwa ubora wake.

Na ni kwa sababu hiyo mkakati wa ICM unathamini matumizi ya Tathmini ya Athari katika Mazingira, ambayo hapo awali ilikuwa haipewi umuhimu unaostahili. Chombo hiki kikitumiwa vyema kitatusaidia kuboresha utekelezaji wa miradi bila kuathiri ustawi ubora wa mazingira ya pwani.

Kupitia Mkakati wa ICM tutaepuka makosa ambayo yana gharama kubwa kiuchumi na kimazingira. Na kupitia ICM tuna fursa nyingi za kuboresha maisha ya wananchi.

Ufugaji viumbebahari unapunguza umasikini

Pwani ya Tanzania ina utajiri mwingi wa maliasili. Lakini wakazi wake ambao ni asilimia 25 ya idadi ya watu nchini, wengi wao ni masikini. Ni masikini kwa sababu maisha yao ya kila siku yanategemea shughuli za uvuvi mdogomdogo na kwa kiasi fulani kilimo duni cha kutumia jembe la mkono.

Wananchi hao huendesha shughuli za uvuvi kwa ajili ya kupata chakula na kwa kiasi kidogo kwa ajili ya kuuza ili kupata fedha kidogo kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao muhimu kama kulipa karo za shule za watoto wao, kununua nguo na kujipatia matibabu.

Hali hii hailingani na utajiri wa asili wa pwani. Na wala halingani na fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo katika maeneo ya pwani. Mojawapo wa fursa za kiuchumi ambayo inaweza kwa kiasi kikubwa kuwanasua wakazi wa pwani katika janga la umasikini linalowakabili ni ufugaji viumbe bahari.

Kufuatana na watalamu wa mazingira na ikolojia ya pwani na bahari ambao kwa zaidi ya miaka minne wamekuwa wakipembua masuala yanayohusiana na ufugaji viumbe bahari chini ya Tanzania Coastal Management Partnership, kuna maeneo mengi katika pwani ya Tanzania ambayo ni mazuri kwa shughuli za ufugaji viumbe bahari. La muhimu ni kuhakikisha shughuli za ufugaji viumbe bahari zinafanywa kwa uangalifu na kwa mipango madhubuti ili kuepuka athari za mazingira na za kiuchumi.

Watalamu hao ambao wameandaa na kuchapisha kitabu cha mwongozo wa ufugaji viumbe bahari kwa ajiri ya wawekezaji, wanabainisha kwamba kuna fursa kubwa kwa ufugaji viumbe bahari kwa uendelevu nchini Tanzania. Kiwango cha ufugaji viumbe bahari kinaweza kuwa katika miradi midogomidogo ya ngazi ya kifamilia au miradi mikubwa ya makampuni.

"Tanzania ina ikolojia nzuri ya pwani ambayo mazingira yake bado hayajaharibiwa, na ambayo yanaweza kutumiwa kufanya miradi ya ufugaji viumbe bahari. Pamoja na ukweli kwamba ufugaji viumbe bahari unahitaji mipango madhubuti na uangalifu mkubwa ili kuepuka athari za mazingira, bado wananchi wa pwani wanaweza kufanya miradi ya ufugaji viumbe bahari kwa uendelevu na kuweza kupambana na umasikini," anaeleza Fatuma Sobo kiongozi wa kikundi cha watalamu kilichoandaa mwongozo huo.

Mwongozo wa ufugaji viumbe bahari ambao umeridhiwa na Idara ya Uvuvi katika Wizara ya Utalii na Maliasili, ni mojawapo wa nyenzo za kusaidia katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani. Mojawapo wa malengo ya mkakati huo ni kuendeleza mbinu kamilifu na endelevu zinazofaa kimazingira za maendeleo ya matumizi makubwa ya kiuchumi ya rasilimali za pwani ili kupata manufaa ya juu kabisa.

Kilimo cha mwani sasa nishughuli ya familia nyingi katika maeneo ya pwani

Ukibainisha changamoto katika miradi ya ufugaji viumbe bahari, mwongozo unaeleza kwamba ufugaji viumbe bahari unakabiliwa na matatizo mengi ambayo kama hayakuzingatiwa na kupewa kipaombele katika utekelezaji, yanaweza kuleta athari nyingi za kimazingira na kiuchumi.

"Kuanzia ngazi ya kiutawala, ufugaji viumbe bahari ni nyanja inayogusa sekta nyingi na hivyo kuhitaji ushirikiano mkubwa wa sekta mbalimbali. Kwa upande wa mazingira ufugaji viumbe bahari unakabiliwa na changamoto ngumu, kwani hufanyika katika maeneo ambayo hukutanisha bahari na nchi kavu, na pia hugusa nyanja nyingine nyingi za kiuchumi," Sobo anafafanua na kuongeza kwamba mwongozo wa ufugaji viumbe bahari utasaidia kuyakabili masuala yote ya msingi yanayozigusa sekta mbalimbali za kiuchumi, mazingira na maendeleo.

Mwogozo wa ufugaji viumbe bahari umekuja wakati muafaka, wakati juhudi za watu wa nje na ndani zinaelekezwa katika ufugaji viumbe bahari. Mbali na mradi wa ufugaji kamba wilayani Rufiji ulioshindwa kuanza kutokana na kutokidhi matakwa ya mazingira, kuna miradi kadhaa ya ufugaji wa kamba inayopangwa na wawekezaji.

Kilimo cha mwani ndicho kinazidi kushamiri nchini. Kilimo hicho kinachofanywa na wananchi wa kawaida kimeongezeka na kuna dalili kwamba kitazidi kuongezeka kadri muda unavyokwenda. Mwaka 1990 kulikuwa na wakulima 2000 ambao walizalisha tani 808 za mwani kavu. Lakini mwaka 1995 idadi ya wakulima iliongezeka hadi zaidi y 20,000, ambao walizalisha tani 6,452.

"Ni matumaini yetu kwamba mwongozo wa ufugaji viumbe bahari utakuwa wa manufaa siyo tu kwa serikali na taasisi zake, bali pia kwa makapuni ya wawekezaji na wakazi wa pwani kwa ujumla. Kwani mwongozo huo ni chombo cha kuhakikisha shughuli zote za ufugaji viumbe bahari zinafanywa kwa uendelevu kwa manufaa ya taifa na maendeleo ya wananchi. Hii ni licha ya kutoa fursa ya kutathmini miradi ya ufugaji viumbe bahari kwa uwazi na ushirikishaji wahusika wote," Sobo anafafanua.

Kufuatana na Sobo, utaratibu uliokuwa unatumika kutathmini na kuruhusu miradi ya ufugaji viumbe bahari ulikuwa na mapungufu mengi ambayo yalitoa mwanya kwa uharibifu wa mazingira, licha ya kuleta khero kwa wawekezaji. "Mwongozo huu ambao serikali imeuridhia unatoa fursa ya kufanya tathmini kwa ufanisi na uwazi, na unalinda maslahi ya wakazi wa pwani wakati huo huo ukihamasisha uwekezaji katika nyanja ya ufugaji viumbe bahari. Nia ni kuwa na miradi inayozingatia ustawi wa mazingira wakati huohuo ikiwanufaisha wananchi na taifa kwa ujumla."

Baada ya kutoa mwongozo huo kuna dalili njema kwamba shughuli za ufugaji viumbe bahari zitaboreka na kuchangia maendeleo ya wananchi na taifa kwa ujumla. Hii, kufuatana na Sobo inatokana na taasisi mbalimbali ambazo ni wadau wakuu wa shughuli za ufugaji viumbe bahari kuridhika na mwongozo huo. Taasisi hizo ni pamoja na Idara ya Uvuvi, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Idara ya Wanyamapori, Kituo cha Uwekezaji (TIC), Idara ya Misitu, Mamlaka ya Bandari, Idara ya Maji na taasisi nyingine ambazo zimeeleza kuwa mwongozo unakidhi mahitaji na maslahi ya kitaifa.

Taasisi hizo ambazo zimekuwa zikikabiliwa na matatizo mengi katika masuala ya ufugaji viumbe bahari zimetoa wito kwa wawekezaji na mamlaka mbalimbali katika ngazi ya kitaifa na wilaya kutumia mwongozo huo katika kuidhinisha na kuanzisha miradi ya ufugaji viumbe bahari ambayo ina fursa nyingi za kukuza uchumi wa taifa na wananchi wa pwani.

Umuhimu wa sayansi katika kulinda rasilimali za pwani

Zuberi Ally ni mkazi wa Mtwara mjini. Maisha yake yote yanategemea uvuvi katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Ana mke na watoto wake watano pamoja na watoto watatu wa marehemu kaka yake aliyefariki miaka mitano iliyopita.

Watoto wake watatu pamoja na wawili wa kaka yake bado wanasoma katika shule za msingi na sekondari. Ili aweze kumudu maisha yake, analazimika kutumia ujuzi na ujanja wake wote ili kupata fedha kwa ajili ya matunzo ya familia yake ikiwa ni pamoja na gharama ya karo ya shule ya watoto hao.

Kwa wakati fulani, anakiri kwamba analazimika kutumia njia haramu za uvuvi kama vile kutumia baruti na nyavu za tundu ndogo ili aweze kupata chochote. "Kurudi nyumbani mikono mitupu ni sawa na uhalifu mwingine. Mtu mwenye familia hatakwepa kutenda uovu huo," anaeleza.

Ally, ni mmoja kati ya maelfu ya wananchi wa Tanzania ambao wanaishi maeneo ya pwani ambao maisha yao yote hutegemea raslimali zipatikanazo pwani na ambao katika harakati za kutafuta maisha na maslahi huharibu mazingira tekechu ya pwani.

Ally, kama wakazi wengine wa pwani anakiri kwamba anatambua kwamba kuvua kwa kutumia baruti au nyavu zenye matundu madogo ni kuvunja sheria licha ya kuchafua mazingira. Hata hivyo, anasema yuko tayari kuachana na uvuvi haribifu huo akipata njia mbadala ya kupata kipato cha kuitunza familia yake.

Vitendo na mwenendo wa Ally vinadhihirisha umuhimu wa Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani. Mkakati huo siyo tu utawaongoza wananchi katika usimamizi na matumizi sahihi ya rasilimali za pwani, bali utajenga mshikamano wa kusimamia na kuendeleza ikolojia muhimu ya pwani.

Ni kwa misingi hiyo kwamba Mkakati wa ICM utatoa kipaombele kwa matumizi ya sayansi kuyasimamia na kuyaendeleza maeneo yenye umuhimu, wakati huo huo ikihakikishwa wananchi wa pwani wanaendelea kwa matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

"Katika pwani kuna maeneo yenye umuhimu wa kipekee wa kiuchumi na wa ikolojia ambayo yanahihitaji mipango maalumu ya usimamizi ili kuepuka migongano katika matumizi. Maeneo hayo ni pamoja na maeneo yenye vitega uchumi na miundombinu muhimu - kama bandari na viwanda, maeneo chepechepe na maeneo yenye miamba ya matumbawe. Mipango inahitajika kuwezesha usimamizi kamilifu ili kuepuka migongano na uharibifu," anaeleza Dk. Gasper Mahika, mratibu wa kikundi cha wanasayansi chini ya Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP)

Akibainisha umuhimu wa sayansi katika usimamizi wa rasilimali za pwani ambazo hutegemewa katika uchumi wa taifa, Mahika anasema katika hali ya sasa kunafanyika makosa mengi katika shughuli za maendeleo pwani kutokana na sababu kadhaa. Anazitaja sababu hizo miongoni mwa nyingine kuwa ni kukosekana kwa taarifa za kisayansi katika kufanya maamuzi ya usimamizi; kukosekana kwa taarifa za kisayansi na ubadilishanaji taarifa miongoni mwa wasimamizi wa pwani; kukosekana kwa utaratibu mzuri wa kuratibu juhudi zinazofanywa katika kufuatila na kupima hali ya pwani; na kukosekana kwa taaluma juu ya mwenendo wa pwani miongoni mwa watumiaji wa rasilimali za pwani.

"Usimamizi wa ikolojia ya bahari na pwani, ambayo mara nyingi huelemewa na shughuli na mahitaji ya watu, hauwezi kupata mafanikio ya maana ikiwa sayansi haitatumika katika kufanya maamuzi. Sayansi haina manufaa tu katika kuelewa jinsi ikolojia inavyofanya kazi, na kuweza kutambua kiwango cha madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya watu, bali pia kutoa taarifa muhimu na kuongoza uandaaji na utekelezaji wa sheria," anaeleza na kuongeza:

Akieleza zaidi, Dr. Mahika anasema kwamba sayansi husaidia kupembua matatizo katika ikolojia ili kuweka mikakati ya usimamizi. Sayansi pia husaidia kubainisha chanzo cha matatizo na madhara katika mazingira. Vilevile sayansi hutoa fursa ya kuielewa mifumoikolojia ili kuweza kuweka sera na mikakati ya kuongoza maamuzi ya usimamizi. Juu ya yote hayo sayansi, ni chombo kizuri cha kufuatilia mienendo ya ikolojia ili kutathmini mafanikio ya sera katika kufikia malengo yake.

"Manufaa na faida za kutumia sayansi katika usimamizi wa mazingira ya pwani ni kwamba sayansi huboresha usimamizi kutokana na utafiti na matumizi ya nyenzo za kisayansi kama ukadiriaji wa madhara katika mazingira kutokana na shughuli za kiuchumi, ufuatiliaji wa hali ya ikolojia na nnyenzo nyingine," anasisitiza Dk. Mahika.

Anaongeza kwamba usimamizi wa mazingira ya pwani ambao hauzingatii sayansi, mara nyingi hupelekea kutokea madhara makubwa katika mazingira na upotevu wa manufaa ya kiuchumi na kiikolojia ya rasilimali za pwani na bahari.

"Hivyo ni kusudio la Mkakati wa ICM kutumia sayansi katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ili kuepuka kuathiri uzalishaji wa ikolojia ya pwani," Dk. Mahika anafafanua na kuongeza;

Anaeleza njia za kuimarisha matumizi ya sayansi katika kusimamia mazingira ya pwani kuwa ni kuboresha ushirikiano miongoni mwa wanasayansi, viongozi, watumiaji wa rasilimali na wananchi. Anazitaja njia nyingine kuwa ni kuwa na taratibu za kuunda na kutekeleza sera na mikakati; na kutenga maeneo ya utafiti katika maeneo ya pwani.

Ni kutokana na haja hiyo kwamba Mkakati wa ICM unaelekeza kuundwa kwa kikundi cha wanasayansi katika muundo wa utekelezaji ICM. Kikundi hicho kitawaunganisha wanasayansi na wasimamizi na kitatoa fursa kwa matumizi ya sayansi katika usimamizi wa maeneo ya pwani.

"Majukumu makuu ya kikundi cha wanasayansi ni pamoja na kukusanya na kusambaza taarifa muhimu za kisayansi. Pia kikundi hicho kitatoa ushauri wa kisayansi ambao utasaidia kuboresha misingi ya usimamizi," anafafanua Dk. Mahika.

Juu ya hayo kikundi cha wanasayansi ambacho kitafanya shughuli zake kwa karibu sana na taasisi nyingine za usimamizi na utekelezaji, kitaelekeza nguvu zake katika ukadiriaji, ufuatiliaji na utafiti ili kubainisha hali halisi na mahusiano baina ya matumizi ya watu na madhara yatokanayo.

Utafiti wa kisayansi ni muhimu katika usimamizi wa mazingira ya pwani. Wanasayansi wakionekana katika mijawapo wa shughuli za utafiti baharini.

Manufaa ya Mkakati wa ICM

Dk. Magnus Ngoile,

Tanzania imedhamiria kuyasimamia na kuyaendeleza mazingira tekechu ya pwani na rasilimali zake. Katika kufanikisha dhamira hiyo, serikali imeamua kuweka na kutekeleza kwa makini Mkakati wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani maarufu kama ICM. Lengo kuu la Mkakati huo ni kuboresha maisha ya wananchi, hasa wakazi wa pwani kutokana na matumizi sahihi ya mazingira ya pwani na rasilimali zake. Katika mahojiano maalum na waandishi wa habari, Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Magnus Ngoile na Kiongozi wa Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP), Jeremiah Daffa, wanabainisha kwanini Tanzania imechagua na kuamua kutumia misingi ya ICM katika kusimamia na kuendeleza mazingira ya pwani na rasilimali zake.

Bw. Jeremiah Daffa

Swali: Tunajua kwamba tumo katika uzinduzi wa Mkakati wa Taifa wa ICM. Mnaweza kutueleza kwa kifupi ICM ni nini?

Jibu: ICM ni kifupisho cha maneno ya Kiingereza; Integrated Coastal Management ambayo tafsiri yake katika Kiswahili ni Usimamizi Kamilifu wa Mazingira ya Pwani.

Usemi usimamizi kamilifu unatokana na maadili ya usimamizi huu ambao unazingatia ushirikishwaji wa wahusika wote katika kupanga na kutekeleza mipango ya usimamizi na utumiaji rasilimali na mazingira ya pwani kwa uwiano na uendelevu.

Ni vizuri ieleweke kwamba jamii za asili zinazoishi pwani, tangu awali zilikuwa na miundo yake ya maisha iliyotilia maanani utumiaji bora wa rasilimali na mazingira yake. Miundo hiyo iliwezesha matumizi endelevu kwa kiasi fulani. Lakini teknolojia ilivyozidi kukua kumekuwepo na mabadiliko makubwa. Na kwa bahati mbaya, mabadiliko hayo, mengi yake yamekuwa ya kuleta uharibifu zaidi katika mazingira.

Hali hii ndiyo iliyopelekea kuanzishwa kwa ICM ambayo sasa inatambuliwa na Umoja wa Mataifa kama chombo ambacho kikitumiwa vizuri kinaweza kuboresha mazingira ya pwani wakati huohuo watu ambao wanategemea rasilimali za pwani, wakipata fursa za kiuchumi na hivyo kuboresha maisha.

Swali: Nani wamefadhili uandaaji wa Mkakati huu na utekelezaji wake utafadhiliwa na nani?

Jibu: Uandaaji wa Mkakati wa ICM umewezeshwa kifedha na kitaalam na serikali ya Marekani kupitia USAID na Chuo Kikuu cha kisiwa cha Rhode. Serikali ya Marekani itaendelea kutoa msaada katika hatua za awali za utekekelezaji Mkakati huo, kabla serikali hajachukuwa jukumu zima la uwezeshaji.

Hata hivyo mashirika na taasisi nyingine za kimataifa zimekuwa zikisaidia kitaaluma na kifedha juhudi za ICM nchini. Kwa mfano huko Tanga, tunasaidiwa na IUCN kupitia serikali ya Uholanzi. IUCN pia inatusaidia huko Rufiji katika Mradi wa Usimamizi wa Mazingira Rufiji (MUMARU). Mikoa ya Kusini yaani Mtwara na Lindi, tunasaidiwa na serikali ya Finland. Pia huko Mtwara katika mradi wa Hifadhi ya Bahari ya Mnazi Bay tunasaidiwa na GEF/UNDP. Huko Mafia, Hifadhi ya Bahari Mafia tunasaidiwa na WWF na serikali za Uingereza na Norway. Na huko Kilwa, tunasaidiwa na mfuko wa Kimarekani wa Pew unaolenga kuanzisha hifadhi. Bila kusahau serikali za Japan na Ufaransa kwa kushirikiana na UNESCO, ambazo zinasaidia ukarabati wa majengo ya kale ya Kilwa.

Azma ya mkakati huu, ni kuunganisha nguvu na mipango mingine endelevu ili kuhakikisha tunaendeleza na kuboresha mazingira ya pwani yetu kwa matumizi ya busara ya rasilimali ili kuongeza uzalishaji. Kwa mfano, kule Tanga kulikuwa na tatizo la uvuvi haramu wa kutumia baruti. Ilifika wakati Tanga walikuwa hawana kabisa samaki kutokana na uvuvi haramu. Baadaye ikaanzishwa vita ya kupambana na wavuvi haramu wa kutumia baruti.

Vita hii iliendeshwa kwa ushirikiano mkubwa na wananchi wenyewe na ilikwenda sambamba na kuwapatia wananchi nyavu mbadala. Badala ya kutumia nyavu zenye macho madogo, walipewa nyavu zenye macho makubwa ambazo hazivui samaki wadogo.

Swali: Je, Zanzibar iko chini ya Mkakati huu?

Jibu: Zanzibar haimo kwenye mkakati huu. Na sababu kubwa za kutokuwamo kwake ni mbili. Kwanza mambo yanayoshughulikiwa na mkakati huu, siyo mambo yanayoangukia katika masuala ya muungano.

Lakini sababu kubwa ya pili ni kwamba Zanzibar wenzetu walitutangulia. Tayari wanao mkakati wao ulioanza mapema.

Swali: Mkakati huu unatekekezwa katika maeneo yapi?

Jibu: Mkakati huu unatekelezwa katika wilaya zote za pwani kuanzia ya Tanga hadi Mtwara. Tulichukua wilaya kwa sababu kule kuna uongozi ulio karibu kabisa na wananchi na wala uongozi wake hauwezi kubadilika badilika na zinaweza kuwa na utendaji bora.

Lakini pia mbali ya kushughulikia wilaya za mikoa ya pwani, bado tunaamini kuwa shughuli za kijamii na kiuchumi zinazofanyika katika mikoa mingine, zinaweza kuwa na athari katika eneo la pwani. Nitatoa mfano, huko nyuma wakati watu wameanza kutumia kwa ufanisi maji ya Mto Ruaha katika bonde la Usangu, matumizi ya maji katika mto huo yalianza kuleta matatizo katika bonde la Rufiji.

Wakati maji yakiwa mengi, Rufiji humwaga maji yake kupitia mito (tributaries) tisa. Lakini wakati maji yakipungua, maji yanaingia kwa kupitia mito saba. Kwa hiyo kama matumizi ya Mto Ruaha yatakuwa mabaya, bila shaka na eneo la pwani litaathirika. Hivyo pamoja na kujishughulisha na mikoa ya pwani, macho yetu yanaangalia eneo pana kuliko hapa.

Swali: Je, ni raslimali gani zinashughulikiwa chini ya mkakati huu?

Jibu: Kwa watu wengi unapozungumzia raslimali za pwani, hudhani kwamba raslimali hizo ni samaki tu. Lakini rasilimali za pwani ni nyingi sana. Labda nianzie na ile ambayo siyo wengi wanaifikiria kuwa raslimali, ambayo ni usafiri wa meli na vyombo vya baharini. Kwa sasa, watu wengi wa pwani wanatumia usafiri wa majini kama usafiri wao mkubwa. Kwa hiyo meli ni mojawapo ya raslimali muhimu kwa usafiri wa majini.

Raslimali ya pili ni utalii. Wote tunajua kuwa utalii wa pwani unaambatana na mambo mengi. Unaambatana na ujenzi wa hoteli kubwa za kitalii. Utalii wa pwani unaambatana na uzamiaji baharini kwa lengo la kuyaona matumbawe ambayo yana mandhari ya kipekee.

Raslimali nyingine ni madini. Bila shaka tunajua kuhusu suala la gesi ya Songosongo. Habari tunazopata ni kwamba hadi ifikapo mwaka 2005, gesi ya Songosongo itakuwa tayari imefika Dar es Salaam. Lakini pia kuna hazina nyingine ya gesi ambayo iko Mnazi Bay. Gesi iliyoko hapa ni nyingi kuliko ile ambayo iko Songosongo.

Kwa bahati mbaya watu wa Msumbiji hawana shida na umeme lakini wangekuwa na tatizo la umeme, tungeweza kutengeneza umeme huko huko Mtwara na kuwauzia watu wa Msumbiji. Hizo ni baadhi tu ya raslimali zilizoko pwani lakini kuna uvuvi, kuna miti ya mikoko na mambo mengine.

Swali: Mkakati huu umejiandaa vipi kulinda mazingira ya pwani ambayo ni tekechu?

Jibu: Ni kweli kwamba maeneo mengi ya pwani ni tekechu. Na misingi ya kuunda Mkakati wa ICM imetokana na kutambua kwamba pwani ni eneo la kipekee katika mazingira ya nchi na katika nyanja nzima ya uchumi na maendeleo. Na kutokana na hali hiyo, Mkakati huu umejianda vilivyo kuyalinda na kuyaendeleza mazingira ya pwani.

Katika utekelezaji wa Mkakati kutakuwepo na mipango na taratibu mahususi za kusimamia, kuhifadhi na hata ikibidi kurejesha hali ya asili ya mazingira ambayo yanakabiliwa na athari mbalimbali aidha za asili au zinazotokana na matumizi ya watu. Kwa mazingira ambayo ni tekechu zaidi yatahifadhiwa na hata ikibidi uwekezaji katika maeneo hayo unaweza kuzuiliwa ili kuepuka madhara makubwa zaidi katika mazingira hayo.

Kwa mazingira mengine, kutakuwa na utaratibu wa wazi usio na kificho wa kuwekeza na kusimamia shughuli mbalimbali. Wahusika wote wakiwemo wananchi wa eneo husika watazijua taratibu hizo na kila mtu atakuwa huru kuangalia kama maeneo hayo yanavurugwa au kuna kukiuka masharti.

Lakini pia, tumeandaa taratibu za uwekezaji na hasa katika ufugaji viumbebahari na utalii wa pwani. Hapo zamani kama tunavyokumbuka, tulipata matatizo ya uwekezaji katika mradi wa kamba kule Rufiji.

Wakati mradi huo unaanzishwa, utaratibu huu ulikuwa haujaanza. Sasa kuna utaratibu ambao umewekwa kwa ajili ya kulinda na/au kuelekeza matumizi endelevu ya maeneo tekechu. Tunatarajia kupata ushirikiano wa wawekezaji katika suala hili ili tuwe na miradi endelevu na yenye kuleta manufaa zaidi kiuchumi na kimazingira.

Tunasema tutakuwa na kazi ya kupunguza madhara katika mazingira yetu. Hatusemi tutaondoa kabisa athari kwani hakuna mradi wowote unaoanzishwa hasa katika maeneo ya pwani ambao hauna athari kwa mazingira. Miradi yote ina athari kwa mazingira.

Swali: Kumekuwapo na utafiti mwingi unaofanywa kuhusu maeneo ya pwani. Lakini kwa bahati mbaya utafiti huu haujaratibiwa na matokeo yake ni kwamba baadhi ya tafiti zinarudiwa. Je, tatizo hili mmeliona? Na kama mmeliona linshughulikiwaje chini ya ICM?

Jibu: Tatizo hili ni kweli tumeliona. Na kweli zipo taasisi nyingi na kila taasisi ilikuwa ikifanya utafiti wake. Lakini baada ya kuanzishwa ICM, tutakuwa na kitengo cha wataalam kitakachoshughulikia suala la utafiti. Tunatambua umuhimu wa kutumia taarifa za kisayansi katika shughuli yoyote ya maendeleo.

Kama mnavyofahamu, mwishoni mwa mwaka juzi, Waziri Ntagazwa alizindua kitabu cha ripoti ya hali halisi ya pwani. Desemba mwaka huu, tunatarajia kutoa ripoti ya pili. Ripoti hizi zinazotengenezwa na watafiti wa hapa nchini zitatupa fursa ya kufuatilia hali ya mazingira na kutupa upeo wa kuchukuwa hatua zinazostahili.

Swali: Unaweza kutueleza sura halisi ya mkakati wenyewe?

Jibu: Katika kitabu cha mkakati tunachozindua leo, kuna Utangulizi: Sura hii ya utangulizi inazungumzia umuhimu wa pwani na kwa nini pwani inapewa nafasi kubwa kama kichocheo cha maendeleo ya nchi yetu.

Lakini pia kuna masuala ya pwani. Ndani ya mkakati huu tunaelezea hali ya mazingira yetu. Tunaangalia uharibifu wa mazingira. Kwa ujumla tunaangalia matatizo yaliyopo.

Mkakati huu unayo mikakati mingine ndani yake na jinsi ya kukabili masuala mbalimbali. Kuna mikakati saba inayohusiana na uondoaji umaskini, matumizi ya sayansi, uwezeshaji na uhamasishaji wa wananchi katika matumizi sahihi ya rasilimali na mazingira ya pwani.

Wataalam wa usimamizi wa mazingira ya pwani wakiwa katika ziara ya uchambuzi wa maswala mbalimbali wakati wa maandalizi ya Mkakati wa ICM

Ushirikishwaji wananchi katika ICM

Ni jambo lisilo na shaka kwamba Mkakati wa Taifa wa Hifadhi Kamilifu ya Mazingira ya Pwani ni mkombozi wa wakazi wa pwani ambao hutegemea bahari na rasilimali zake kwa chakula na maisha. Mkakati wa ICM unakusudia kuhifadhi na kulinda mazingira na rasilimali za pwani kwa ajili ya kuboresha maisha ya wakazi wa pwani.

Pia ni jambo lisilo na shaka kwamba ICM inalenga kuendeleza fursa za kiuchumi ambazo zitachangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa. Katika matarajio yake, Mkakati wa ICM unalenga kuwepo ushirikiano kamilifu kati ya serikali na wadau wote katika jumuiya ya Watanzania, wakiwemo watumiaji rasilimali, sekta binafsi, wanasayansi, tasisi za utafiti na tasisi nyingine, zikifanya juhudi za kupata mafanikio.

Hivyo, hatua ya serikali ya kuandaa na kuweka Mkakati wa ICM, ni hatua ya busara . Ni utaratibu mzuri chini ya Sera ya Taifa ya Mazingira, unaoziunganisha sekta mbalimbali na kuweka mshikamano wa kuyatumia mazingira ya pwani kwa uendelevu.

Na kwa misingi hiyo Mkakati wa ICM unabainisha umuhimu wa pekee wa kusaidia juhudi za kupanga utekelezaji wa shughuli za pwani katika ngazi ya wilaya na vijijini. Hii siyo tu inalenga kusaidia katika uendelevu wa mazingira ya pwani, bali pia kuboresha maisha ya watu ambao hutegemea rasilimali za pwani kwa kipato na chakula.

Kwa kutumia Mkakati wa ICM wananchi katika ngazi ya wilaya na vijiji wataweza kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo na usimamizi wa mazingira. Hii ni pamoja na kubainisha masuala, kubuni mikakati ya kuyashughulikia na kutekeleza mikakati hiyo kwa lengo la kupata maendeleo endelevu na ustawishaji endelevu wa vyanzo vya rasilimali.

Upangaji wa shughuli za ICM katika ngazi ya wilaya na vijiji, kufuatana na Lewis Nzali ambaye ni mratibu wa kikundi cha wataalamu waliotengeneza Mkakati wa ICM, ni njia bora ya kuweza kuyatanzua matatizo ya usimamizi na ya mazingira yanayobainishwa.

"Manufaa ya utaratibu huu ni kwamba masuala mbalimbali huweza kutatuliwa kwa ushrikishwaji wa wadau wote ambao wanahusika katika kupanga na kutekeleza majukumu mbalimbali", anaeleza Nzali.

Kufuatana na Nzali, utaratibu huu husaidia kugawana majukumu na mamlaka katika usimamizi wa maliasili za pwani. "Utaratibu huu huwapa mamlaka na sauti wananchi katika kubainisha fursa na matatizo, na hatimaye kupanga hatua na mikakati ya kutatua matatizo yanayojitokeza kwa kushirikiana na maafisa wa halmashauri za wilaya. Hivyo, upangaji na utekelezaji shughuli za ICM wilayani na vijijini ni kipimo kizuri cha mafanikio ya ICM".

Licha ya kutoa fursa na njia muafaka za kuziimarisha halmashauri za wilaya ili ziwajibike kwa wananchi, upangaji wa shughuli za ICM pia huchangia katika utekelezaji wa Programu ya Urekebishaji Serikali za Mitaat ambayo inalenga kuzipa halamashauri za wilaya madaraka ya kusimamia shughuli za maendeleo, ukiwemo usimamizi wa maliasili.

Akisisitiza kwamba mafanikio ya utekelezaji wa Mkakati wa ICM utatokana na upangaji mzuri wa shughuli za ICM katika ngazi ya wilaya na vijijini, Nzali anataja manufaa ya utaratibu huu kuwa ni pamoja na:

- Kuwapa mamlaka na sauti wote wanaohusika katika kupanga na kutekeleza mipango iliyokusudiwa
- Utekelezaji wa hatua zinazolenga tatizo lililochunguzwa na kuchambuliwa kwa makini
- Ufuatiliaji wa matokeo ya hatua zilizochukuliwa
- Upimaji wa mara kwa mara maendeleo kutokana na hatua zilizochukuliwa - na kama kuna ulazima kuweka programu maalumu ya utekelezaji na ufuatiliaji

Chombo kikuu cha kufanikisha upangaji wa shughuli za ICM ni kikundi kinachoundwa na wataalamu kutoka katika sekta mbalimbali na taasisi zikiwemo sekta ya binafsi, wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali.

"Kikundi hiki hubeba jukumu la kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli kwa kuwahusisha kwa karibu wananchi katika eneo linalohusika. Kwa kufuata misingi ya ICM, kikundi hubainisha na kuyapima masuala yanayohitaji kushughulikiwa kabla ya hatua kuchukuliwa," anafafanua Nzali.

Akijibu swali kuhusiana na ufanisi wa upangaji kwa kutumia misingi ya ICM, Nzali anaeleza kwamba wilaya za Pangani na Bagamoyo zinaanza kupata matunda ya utaratibu huu. "Wilaya zote mbili hivi sasa zinayatatua masuala kadhaa yanayohusiana na matumizi yasiyoendelevu ya rasilimali za pwani. Inatarajiwa kwamba kadri wilaya hizo zinavyoendelea kuyakabili masuala mbalimbali, taratibu zitafanywa kuweza kupata ufumbuzi wa matatizo na vitendo visivyokuwa endelevu."



Mafanikio ya usimamizi wa mazingira ya pwani mkoani Tanga yanatokana na ushirikishwaji wa wananchi. Ktika picha hii wananchi wa Kipumbwi wakipanga mipango ya utekelezaji.

Utalii wa pwani muhimu kwa maendeleo

Tanzania imebahatika kuwa na pwani nzuri inayovutia na ambayo ina fursa nyingi za utalii. Utalii wa pwani ukiendelezwa kikamilifu ni chanzo kimojawapo cha kukuza uchumi wa taifa.

Lakini pamoja na mandhali yake ya kuvutia, pwani ya Tanzania haijaendelezwa kiasi cha kutosha na kuifanya iwe ni kuvutio kikuu cha watalii. Karibu pwani yote ya urefu wa kilomita 800 kutoka Tanga hadi Mtwara, imejaa vivutio mbalimbali ambavyo kama vingeendelezwa vingekuwa ni chanzo kikubwa cha fedha za kigeni ambazo zingeingizwa na watalii.

Vivutio hivyo ni pamoja na fuko murua, magofu ya kale na majengo mengine ya kihistoria, bila kusahau utamaduni wa wakazi wa pwani. Pia katika maeneo ya pwani kuna maeneo ya hifadhi ya wanyama pori, ambayo yana mvuto wa pekee kwa wageni.

Changamoto inayoikabili Tanzania ni kuboresha sekta ya utalii wa pwani ambao utaliletea faida taifa lakini ambao hauna madhara kwa mazingira na utamaduni wa wakazi wa pwani. Changamoto nyingine ni kuzingatia kwamba utalii hauziathiri sekta nyingine.

"Nia ya serikali ni kuwa na utalii ulio endelevu katika hali zote. Kusudio siyo utalii unaoleta mapato mengi tu, bali utalii usiodhuru ustawi wa mazingira, usiokiuka maadili ya tamaduni za wakazi wa pwani, na ambao hausababishi madhara au migongano katika shughuli za sekta nyingine", anaeleza Ildefonce Masekesa, mratibu wa kikundi cha wataalamu wa masuala ya utalii chini ya Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP)

Ukiwa miongoni mwa sekta muhimu za uchumi nchini, utalii huchangia asilimia 13% (hasa kutokana na utalii katika mbuga za wanyama zilizopo kasikazini), katika pato la taifa, na hutoa ajira kwa zaidi ya watu 150,000.

Lakini kutokana na utajiri mkubwa wa raslimali na maliasili nchini, utalii bado haujatumiwa vizuri ili uchangie zaidi pato la taifa. Na ni kwa kutambua hilo, kwamba serikali inafanya juhudi kuimarisha utalii wa pwni ili ulete manufaa bora zaidi kwa serikali na wananchi.

Hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa. Mojawapo ni utayarishaji wa Mpango wa Taifa wa Utalii, ambao unatoa mwongozo kwa wawekezaji wa nje na ndani. Mpango huo unabainisha maeneo yanayofaa kwa uwekezaji katika utalii wa pwani.

Utekelezaji wa mpango huo tayari umeanza kuzaa matunda. Hoteli za ufukoni zimeanza kukarabatiwa na maeneo ya ujenzi wa hoteli mpya yamenza kugawiwa kwa wawekezaji. Hali inaanza kuleta matumaini hasa katika maeneo yenye mvuto wa pekee. Maeneo hayo ni pamoja na wilaya ya Kilwa, Hifadhi ya Saadani, Pangani, Bagamoyo, Mtwara - ambako imeanzishwa Hifadhi ya Bahari ya Mnazi Bay, na Hifadhi ya Bahari ya Mafia.

Tayari wataalamu wa masuala ya utalii wamefanya utafiti yakinifu, na kuchapisha Mwongozo wa Kuendeleza Utalii wa Pwani. Utalii wa pwani ni mojawapo wa nyanja inayolengwa kuboreshwa katika utekelezaji wa Mkakati wa ICM.

"Ni matumaini ya serikali kwamba kupitia kanuni za ICM, Tanzania itaweza kuimarisha shughuli za utalii. Mkakati huo wa ICM unaelekeza uendelezaji wa utalii wa pwani unaozingatia ustawi wa mazingira, na unaotoa kipaombele kwa maslahi ya wadau wote," anafafanua Masekesa.

Katika utaratibu unaokusudiwa, kufuatana na Masekesa, uendelezaji wa utalii wa pwani utaendana na juhudi za taifa za kukuza uchumi zikiwemo Programu ya Kurekebisha Serikali za Mitaa, sheria mpya ya ardhi, Mpango wa Taifa wa Utalii, sheria ya Hifadhi za Bahari, Mkakati wa Kuodoa Umasikini na Mkakati wa Taifa wa ICM.

Hatua za kuimarisha na kuboresha utalii wa pwani zimeanza kuchukuliwa: Hatua hizo ni pamoja na kuchambua na kuchapisha masuala yanayohusiana na utalii endelevu wa pwani na kutoa mwongozo wa serikali katika uendeshaji utalii endelevu wa pwani. Mwongozo wa Utalii Endelevu wa Pwani unalenga kuwasaidia na kuwaelekeza wawekezaji katika kufuata maadili na njia endelevu za kuendesha shughuli za utalii wa pwani.

Hata hivyo, bado kuna kazi kubwa, hasa katika kuboresha miundombinu ikiwemo ya mawasiliano na barabara, ili kuufanya utalii wa pwani ushamiri na kuleta manufaa yanayostahili. Matumaini kidogo yaliyopo ni hatua zinazochukuliwa sasa zikiwemo za ukarabati wa barabara ya Dar es Salaam - Mingoyo, ukarabati wa magofu ya Kilwa na Bagamoyo, na uanzishaji wa Hifadhi ya Taifa ya Saadani na Hifadhi ya Bahari ya Mnazi Bay.

Hatua zaidi zinatarajiwa kutokana na utekelezaji Mkakati wa ICM ambao katika utekelezaji wake mipango ya usimamizi wa utalii katika maeneo muhimu itatayarishwa. Mpaka sasa umetayarishwa na kuchapishwa Mwongozo wa Kuendeleza Utalii wa Pwani ambao umeridhiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara ya Maliasili na Utalii. Madhumuni ya mwongozo huo ni kuhakikisha kwamba uendeshaji wa utalii wa pwani unazingatia uendelevu wa maeneo husika na watu waliomo katika maeneo hayo. Hii ni kutokana na ukweli kwamba shughuli za utalii zinaweza kuziathiri sekta nyingine na hata wenyeji wa maeneo husika.



Boma la Mikindani ambalo limekarabatiwa na kunakshiwa kwa matumizi ya hoteli ya kitalii